

Kumbuka

Unaweza kupunguza utegemezi wa mbolea ya dukani kwa kukuza mimea kama kunde ikiwa mbolea.

Matokeo

Mseto wa mimea aina ya kunde pamoja hutoa kiwango cha kilo 800-1,600 kwa kila ekari za majani baada ya kuoza hutoa kilo 20-36 za nitrojeni.

Kiwango hiki ni sawa na kilo 80-150 za C.A.N au ngunia 1.5 hadi 3 za C.A.N.

Mahindi huhitaji kilo 24 za Nitrojeni kwa kila ekari (kama ngunia 2 za CAN) na kwa hivyo mimea hii kwa mtindo huu huipa mahindi nitrojeni ya kutosha.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Gitaari, N

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Embu

S.L.P. 27 Embu


Simu: (+254 068) 31116/31873

Baruapepe: kariembu@salpha.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 6 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Tumia mbolea ya mimea ya jamii ya mikunde kupunguza mbolea ya kununua



Utangulizi

Mbolea ya mimea ya mikunde ni majani yanayokuwa na nitrojeni katika matawi wa mihimili yake (majani).

Nitrojeni hii na virutibishi vingine huachiliwa wakati mimea inapooza.

Mifano ya majani hayo ni *Mucuna* (upupu), mchangani na '*Crotalaria*' miongoni mwa mingine.



Mucuna



Crotalaria

Namna ya kutumia mbolea ya kijani kibichi kwenye mahindi

Hatua 1

Panda mbegu za mahindi umbali wa sentimita 75 kwa 50 au umbali mwingine unaoruhusiwa.

Hatua 2

Panda mstari mmoja wa mimea ya aina hiyo (*Mucuna* au *Crotalaria*) kati ya mistari miwili ya mahindi.

- Panda *Mucuna* kati ya sentimita 2-3 kwa kila sentimita 30.
- Chimbua *Crotalaria* mashimo kwa kilo 15 kwa ekari.

Panda mimea hivyo ilivyo kama kunde siku moja au wiki 2 baada ya mahindi na usitumie mbolea ya nitrojeni kwa majani hayo ya kunde.



Mseto wa mahindi na *Crotalaria* shambani

Hatua ya 3

Mahindi yanapokomaa vuna mahindi na mihimili yake na uache mimea mchangani.

Hatua ya 4

Ng'oa au ukate mbolea ile ya kunde baada ya kuvuna mahindi.



Ung'oaji wa *Crotalaria* iliyochanganywa na mimea

Tumia masalio kama kifunikiro kisha uchanganye katika mchanga kabla ya kupanda katika msimu ujao.